JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA

Tarehe: 30/06/2021

# TANGAZO LA KAZI KWA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mafia anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi za mkataba kwa Kada mbalimbali kama zinavyojionesha hapa chini.

1. **MSAIDIZI WA HESABU (NAFASI 3)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe Mtanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 40
- Awe amehitimu stashahada (Diploma) ya uhasibu kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali au cheti cha ATEC II inayotolewa na NBAA
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha Nne.

**MSHAHARA:**

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA MSHAHARA WA SERIKALI TGS C SAWA NA TSH. 525,000/=

**KAZI ZA KUFANYA:**

i. Kutunza daftari la fedha
ii. Kutunza nyaraka za hati za malipo
iii. Kuingiza mapato na matumizi kwenye vitabu vya fedha
iv. Kuandika taarifa mbalimbali za fehda zinazopokelewa
v. Kukusanya mapato ya Halmashauri kwa mashine za POS mashine
vi. Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa na mkuu wa kazi

MKURUGENZI MTENDAJI (W
HALMASHAURI YA WILAYA
01 JUL 2021
P. O. Box 85
MAFIA

Scanned with CamScanner

## 2. AFISA UVUVI MSAIDIZI (NAFASI 2)

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne au sita (form 4 au 6)
- Awe na umri kati ya miaka 18 - 40
- Awe na Stashahada (Diploma) ya uvuvi au uhifadhi wa samaki na masoko (Fish Processing and Marketing) kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali

**MSHAHARA:**

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA MSHAHARA WA SERIKALI TGS C SAWA NA TSH. 525,000/=

**KAZI ZA KUFANYA:**

I. Kukusanya takwimu za uvuvi
II. Kuandaa taarifa za uvuvi
III. Kutoa ushauri juu ya uvuvi,uhifadhi wa samaki na mbinu za usambazaji na uhifadhi wa mazao ya bahari
IV. Kutoa elimu ya ufugaji na uvuvi wa samaki
V. Kukusanya mapato katika vyanzo vya uvuvi kwa kuzingatia sheria za uvuvi
VI. Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa na mkuu wa kazi

## 3. NAHODHA WA BOTI (NAFASI 1)

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Awe na umri kati ya miaka 18 – 40
- Mwenye cheti cha unahodha na uvuvi (master fishermen) atapewa kipaumbele

**MSHAHARA:**

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA SERIKALI TGS B SAWA NA TSH. 390,000/=

MKURUGENZI MTENDAJI (W
HALMASHAURI YA WILAYA
01 JUL 2021
P. O. Box 85
MAFIA

Scanned with CamScanner

**KAZI ZA KUFANYA:**

I. Kubuni na kuunda zana za usimamizi wa uvuvi baharini
II. Kongoza na kuendesha boti
III. Kufanya shughuli za uvuvi katika boti
IV. Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa na mkuu wa kazi

**4. AFISA BIASHARA MSAIDIZI (NAFASI 1)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Awe na stashahada (Diploma) ya biashara,usimamizi wa masoko,uchumi kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali

**MSHAHARA:**

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA SERIKALI TGS B SAWA NA TSH. 390,000/=

**KAZI ZA KUFANYA:**

I. Kuandaa taarifa za biashara kwa ajili ya mipango ya Halmashauri ya Wilaya
II. Kukusanya na Kuandaa takwimu zinazohusiana na biashara
III. Kuandaa na kusimamia kanzidata za biashara za wilaya
IV. Kusimamia na kukusanya mapato katika vyanzo vya biashara
V. Kukusanya takwimu kutoka kwa wafanyabiashara
VI. Kutoa ushauri wa kibiashara kwa timu ya Menejimenti ya wilaya
vii. Kukusanya na kuunganisha takwimu na nyaraka za sera za biashara na sheria za biashara Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa na mkuu wa kazi
viii. Kufanya kazi nyingine kama utakavyopangiwa na mkuu wa kazi

MKURUGENZI MTENDAJI (W
HALMASHAURI YA WILAYA
01 JUL 2021
P. O. Box 85
MAFIA

Scanned with CamScanner

## 5. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 3)

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Awe na leseni ya daraja C1- C3 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha ufundi stadi (VETA) au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II (Drive Test II) watapewa kipaumbele

**MSHAHARA:**

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA SERIKALI TGS B SAWA NA TSH. 390,000/=

**KAZI ZA KUFANYA**:

I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini usalama wa gari
II. Kufanya matengenezo madogo madodo ya gari
III. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika daftari la safari (Log Book)
IV. Kufanya usafi wa gari
V. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
VI. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
VII. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

a) Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
b) Mwombaji lazima aambatanishe cheti cha kuzaliwa
c) Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba za simu pamoja na majina na anuani za wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika
d) Maombi yote yaambatane na barua ya maombi,nakala ya vyeti vya taaluma,nakala ya cheti cha kidato cha nne au sita kilicho halali,nakala ya vyeti vya kuhitimu mafunzo

MKURUGENZI MTENDAJI (W
HALMASHAURI YA WILAYA
01 JUL 2021
P. O. Box 85
MAFIA

Scanned with CamScanner

e) Mwombaji aambatanishe picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni zenye rangi kwa muono wa nyuma (Background)

f) Testimonials,Provisional results,statement of results,hati za matokeo bila ya kidato cha nne au sita

g) Waombaji wakazi wa Wilaya ya mafia wanahimizwa kuomba zaidi

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 14 JULAI 2021 SAA 2 ASUBUHI**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Mafia,**
**S.L.P 85,**
**MAFIA.**

Limetolewa na ;

**E.C. MAPUNDA,**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA MAFIA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W
HALMASHAURI YA WILAYA
01 JUL 2021
P. O. Box 85
MAFIA

Scanned with CamScanner